BUKU LA 5
Salamu kwa Wilaya ya Shule za Kaunti ya DeKalb,

Tuko katika siku za mwisho za Kurudi Shuleni za 2020. Kuna furaha inayoendelea katika wilaya yetu tunapokuwa tukipanga mwanzo wa ufanisi wa mtandaoni na mwaka wa ajabu wa masomo!

Mpango wa Mkakati wa Wilaya ya Shule za Kaunti ya DeKalb unatumika kama mpango wetu wa kuhakikisha kwamba wilaya yetu inakuwa chaguo nambari 1 kwa familia zote za DeKalb na unawaweka wanafunzi wote kwa Njia ya Mustakabali wao Wanaopendelea. Maeneo ya Lengo Letu la Mkakati ni:

Ufanisi wa Wanafunzi kwa Usawa na Nafasi Sawa
Kuwahusisha na Kuwasiliana na Washikadau
Ubora wa Wafanyakazi
Utamaduni na Hali ya hewa
Ubora wa Shirika
Vituo
Ninatazamia kutumia jarida langu la kila wiki kushiriki maendeleo haya mazuri katika maeneo yetu ya malengo, na shughuli zangu za Siku 100 za Kwanza. Kwa maelezo zaidi kuhusu mpango wetu wa mkakati, tembelea https://www.dekalbschoolsga.org/superintendent/strategic-plan/.

Ufanisi wa Wafanyakazi (Mpango wa Mkakati Lengo la III)

Wiki hii nilikuwa na nafasi ya kuunganika na viongozi wetu wa wilaya ili kuhakikisha kwamba tuko kwenye njia sahihi, kuanzia usambazaji wa vifaa hadi nafasi za maendeleo ya kitaaluma kwa wafanyakazi wetu. Tulianza Taasisi yetu ya Mtandaoni ya Maendeleo ya kitaaluma mnamo Agosti 5-7, 2020. Taasisi hii iliwapa wafanyakazi wetu wa shuleni mafunzo mwafaka ya mtandaoni na mazoezi ya mafunzo ili wanafunzi wetu wahisi wanahusishwa na wanawezeshwa kusoma na kufikia uwezo wao mkubwa. Asante, walimu, walimu wakuu, na wafanyakazi kwa kazi yenu ngumu.

Mawasiliano, ushirikiano, na mshikamano ndio mada kuu zinazoibuka wakati wa mkutano wangu wa kila wiki wa baraza la Wasimamizi. Kwa kuongezea mipango yetu ya Kurudi Shuleni, tumekuwa tukichukua muda tukijadili inamaanisha nini kuongoza wakati wa matatizo na mabadiliko. Yafuatayo ni baadhi ya makala ya kusoma tuliyoyachunguza:

The Resilient Leader – Educational Leadership by Elle Allison

www.ascd.org/publications/educational-leadership/dec11/vol69/num04/The-Resilient-Leader.aspx

First and Second Order Change in Education and Its Implications for Future Directions by Peter Zsebik

http://www.questconference.ca/wp-content/uploads/2018/05/2009ZsebikArticle.pdf

Leading Through Crisis – 8 Tips for Navigating Turbulent Times
by John Taylor

https://www.randstadrisesmart.com/blog/leading-through-crisis-8-tips-navigating-turbulent-times

Student Success with Equity and Access (Strategic Goal I) &
Stakeholder Engagement and Communication (Strategic Plan Goal II)

Nimehimizwa sana na wanajamii wazuri na waliojitolea wa Kaunti ya DeKalb na Mji wa Atlanta. DCSD inatambua kwamba hatuwezi kukidhi mahitaji yote changamani ya wanafunzi, familia na jamii zetu peke yetu, na kwa hivyo ni lazima tushirikiane na familia zetu na viongozi wa jamii kuchapuza ufanisi wa wanafunzi. Hii ni kweli hasa katika nyakati hizi zenye changamoto, huku tuking'ang'ana kuangamiza mwanya wa kidijitali.

Wilaya yetu inazungumza lugha 178 na ina jamii mbalimbali. Tunatafuta njia za ziada za kusheherekea utofauti wetu na kutambua mahitaji ya kipekee ya kila moja ya jamii zetu. Wiki hii nilikuwa na mkutano na Wanafunzi wazuri Wanaojifunza lugha ya Kiingereza wa K-12. Kundi hili la wazazi, walimu, viongozi wa jamii, na mawakili lilitoa maoni ya thamani na mapendekezo ya kuunga mkono ELL yetu na wanafunzi na wanafamilia wa wahamiaji wapya. Asante, tena, kwa kundi hili lililochukua muda wa kukutana na mimi na kushiriki maoni kuhusu jinsi ya kuboresha mawasiliano na familia, usambazaji wa chakula, n ufikiaji sahihi wa intaneti kwa wanafunzi wetu.

Nilihudhuria pia Mkutano wa Town Halll wa Kurudi Shuleni wa Kaunti ya DeKalb uliopangwa na Kamishna Lorraine Cochran-Johnson. Hili lilikuwa tukio nzuri sana na kwa kweli nina furaha kuungana na wengine katika wilaya yetu na jiji la Atlanta ambao pia wanatetea watoto. Kwa wale wote waliohudhuria tafadhali mjue kwamba nilisikia maswali na hoja zenu na ninatazamia kutoa majibu. Kwa kweli tuko bora tukiwa pamoja na kwa pamoja tutatoka kwenye janga hili la kimataifa tukiwa wenye nguvu zaidi kama DeKalb moja.

Learn4Life (L4L), Metro Atlanta Regional Education Partnership, na mimi tulikutana kujadili ahadi yetu ya kuelimisha vijana wetu na kuandaa kizazi kifuatacho cha viongozi na raia. Shirika hili linajumuisha wilaya za shule, jamii, biashara, na mashirika yasiokuwa ya faida na yanawezeshwa na imani yetu ya pamoja kwamba watoto wetu wanahitaji nafasi ya kufikia uwezo wao.

Ubora wa Utaratibu (Eneo V la Lengo)

Mnamo Alhamisi, nilikuwa na nafasi ya kutembelea Idara ya Rasilimali Watu na Mkuu wa Muda wa Rasilimali Watu Bi. Linda Woodard. Kama tujuavyo, Rasilimali Watu ndio uhai wa kuwaajiri wafanyakazi walio na sifa za juu na kukuza na kudumisha vipaji bora. Tunagundua kwamba ufanisi wa wilaya ya shule zetu huanza na Idara yetu ya Rasilimali Watu. Ninaangalia chati yetu ya utaratibu kwa karibu ili kuhakikisha tuna muundo wa ufanisi.

Kwa sababu usalama na maslahi ya wanafunzi na wafanyakazi ndio kipaumbele chetu nambari moja kwa timu yetu, tulipanga mkutano wa Wanariadha wa Town Hall ili kushughulikia baadhi ya hoja zinazoenea kuhusu jinsi COVID-19 imeathiri wanafunzi wetu wanariadha na michezo katika wilaya. Asante kwa timu yangu na mwenzi Dkt. Sandra Ford kwa kushiriki kwenu. Ikiwa uliikosa, unaweza kuitazama kwenye video za TV ya Shule za DeKalb: https://view.earthchannel.com/PlayerController.aspx?&PGD=dekalbschga&eID=781.

Tukiwa na wiki moja iliyosalia, ninakupa jukumu la kujiandaa kiakili kwa mwaka mzuri wa masomo. Tukiwa bado katikati mwa nyakati hizi zenye changamoto, kuwa na mawazo mema, ongea maneno ya himizo, na ujue kwamba ninafanya kazi kwa bidii pamoja na nyinyi. Kuna methali ya Kihaiti ninayoipenda, “Kwa mikono mingi, mzigo unakuwa mwepesi.” Kuweni na wikendi njema!

Shabiki wenu #1,

Cheryl Watson-Harris, Msimamizi